# Ukweli Kuhusu Kifua Kikuu

***Kifua Kikuu Kinaweza Kutibika***

## Kifua kikuu ni nini?

''TB'' ni kifupisho cha ugonjwa unaoitwa kifua kikuu. Kifua kikuu huenezwa kwa njia ya hewa kutoka kwa mtu mmoja kwenda mwingine. Viini vya kifua kikuu hupitishwa hewani wakati mtu ambaye nana **ugonjwa wa kifua kikuu** cha mapafu au koo anapokohoa, kuzungumza, kucheka, kuimba, au kupiga chafya. Mtu yoyote aliye karibu na mtu mwenye **ugonjwa wa kifua kikuu** anaweza kuvuta hewa ya viini vya kifua kikuu kwenye mapafu yake.

Viini vya kifua kikuu vinaweza kuishi kwenye mwili wako bila kukufanya uwe mgonjwa. Hii inaitwa **maambukizi ya kifua kikuu kisichoonekana**. Hii inamaanisha kuwa una viini vya kifua kikuu vilivyolala mwilini mwako. Viini vilivyolala haviwezi kuambukiza mtu mwingine. Hata hivyo, ikiwa viini hivi vitaamka au kuwa hai kwenye mwili wako na kuongezeka, unaweza kuwa na **ugonjwa wa kifua kikuu**.

Pindi viini vya kifua kikuu vinapokuwa hai (na kuongezeka mwilini mwako) hii inaitwa ugonjwa wa kifua kikuu. Viini hivi mara nyingi hushambulia mapafu. Vinaweza pia kushambulia sehemu nyingine za mwili, kama vile figo, ubongo na uti wa mgongo. Ugonjwa wa kifua kikuu utakufanya kuwa mgonjwa. Watu wenye ugonjwa wa kifua kikuu wanaweza kusambaza viini kwa watu wanaotumia muda nao pamoja kila siku.

Ikiwa **ugonjwa wa kifua kikuu** upo kwenye mapafu yako, unaweza:

- kukohoa sana,
- kukohoa kamasi au makohozi (''yanayotoka kwenye mapafu''),
- kukohoa damu, au
- kuwa na maumivu ya kifua unapokohoa.


**MARA ZOTE UNAPASWA KUZIBA MDOMO WAKO unapokohoa!**

Ikiwa una **ugonjwa wa kifua kikuu**, unaweza pia:

- kujisikia dhaifu,
- kupoteza hamu ya kula,
- kupungua uzito wa mwili,
- kuwa na homa, au
- kutoka jasho kwa wingi wakati wa usiku.

Hizi ni dalili za **ugonjwa kifua kikuu**. Dalili hizi zinaweza kuwepo kwa wiki kadhaa. Bila matibabu, zinaweza kuwa mbaya zaidi.

Ikiwa utapata **ugonjwa wa kifua kikuu** kwenye sehemu nyingine ya mwili, dalili zitakuwa tofauti. Ni daktari pekee anaweza kukwambia ikiwa una **ugonjwa wa kifua kikuu**.










Imechukuliwa kutoka CDC

# Ukweli Kuhusu Kifua Kikuu: *Kifua Kikuu Kinaweza Kutibika*

## Nitajuaje ikiwa nina kifua kikuu kisichoonekana au ugonjwa wa kifua kikuu?

Ikiwa umekuwa karibu na mtu ambaye ana **ugonjwa wa kifua kikuu**, unapaswa kwenda kwa daktari wako au idara ya afya kwenye eneo kwa ajili ya vipimo.

Kuna vipimo viwili ambavyo vinaweza kutumika ili kusaidia kugundua **maambukizi ya kifua kikuu** kisichoonekana: kipimo cha ngozi cha kifua kikuu au kipimo cha damu cha kifua kikuu. Kipimo cha ngozi hutumika mara nyingi. Sindano ndogo hutumika kuweka nyezo ya kupimia, ambayo huitwa tuberculin, chini ya ngozi. Ndani ya siku 2-3, unaweza kurudi kwa mfanyakazi wa huduma za afya ambaye ataangalia kama kuna mwitikio kwenye kipimo. Katika matukio mengine, kipimo cha damu cha kifua kikuu kinatumika kwa **maambukizi ya kifua kikuu**. Kipimo hiki cha damu kinapima jinsi mfumo wa kinga wa mtu unaitikia viini ambavyo husababisha kifua kikuu.



Kipimo cha kifua kikuu cha ngozi

Vipimo vingine vinahitajika ili kuonyesha ikiwa una **ugonjwa wa kifua kikuu**. Eksirei ya kifua chako inaweza kuonyesha ikiwa kuna uharibifu wa mapafu yako kutokana na kifua kikuu. **Ugonjwa wa kifua kikuu** unaweza kuwa ndani ya mapafu yako. Makohozi (yanayotoka kwenye kifua) unayokohoa yatapimwa kwenye maabara ili kuangalia ikiwa viini vya kifua kikuu vipo kwenye mapafu yako.

Ikiwa **ugonjwa wa kifua kikuu** upo kwenye mapafu au koo lako, unaweza kuwaambukiza familia au rafiki zako. Unaweza kuwa mgonjwa wa **ugonjwa wa kifua kikuu**. Unaweza kutengwa na watu mpaka ambapo hutaweza kusambaza viini vya kifua kikuu. Hii huenda isiwe kwa muda mrefu, ikiwa utatumia dawa zako kama ulivyoelekezwa na mtoa huduma za afya.



Kipimo cha damu cha kifua kikuu

## Je kifua kikuu kinatibika?


Ikiwa una **maambukizi ya kifua kikuu**, unahitaji dawa ili kuzuia kupata **ugonjwa wa kifua kikuu** baadae. Hii inaitwa matibabu ya "kinga".

**Ugonjwa wa kifua kikuu** unaweza pia kutibika kwa kutumia dawa. Ikiwa una **Ugonjwa wa kifua kikuu**, ni muhimu kuwa umalize dawa zako, na utumie kama ulivyoelekezwa. Ikiwa utaacha kutumia dawa zako mapema sana, utakuwa mgonjwa tena. Ikiwa hukutumia dawa kwa usahihi, viini ambavyo bado vipo hai vinaweza kuwa vigumu kutibika kwa dawa hizo. Inachukua angalau miezi sita na huenda muda mrefu zaidi mpaka mwaka mmoja kuua viini vya kifua kikuu.

Ni muhimu kuwa utumie dawa zako kama ilivyopendekezwa na daktari.



Dawa za kifua kikuu



**Linda familia na marafiki zako dhidi ya kifua kikuu - tumia dawa zako ZOTE za kifua kikuu!**